# JARIDA LA JANUARY 2025

## KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## MKUU WA WILAYA YA KYELA AFANYA KIKAO NA WATUMISHI IDARA YA ELIMU

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe.Josephine Manase amefanya kikao na Watumishi Idara ya Elimu Wilaya ya Kyela katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmshauri tarehe 10/1/2024.

Miongoni mwa waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na kamati ya Ulinzi na Usalama,Watumishi Idara ya Elimu, Watendaji Kata, Taasisi za Serikali ikiwemo NHIF na STAMICO,

Kikao hicho kimeambatana na ugawaji wa Zawadi kwa Walimu na Wanafunzi waliofanya vizuri katika Mitihani yao ya kidato cha Sita,Kidato cha Nne, Kidato cha Pili pamoja na Darasa la Saba na Darasa la Nne kwa mwaka 2023/2024 kwa lengo la kuhamasisha jitihada za ufaulu mzuri kwa Wanafunzi.

Akizungumza mbele ya wadau wa Elimu Mhe. Mkuu wa Wilaya amewataka Wakuu wa Shule za Sekondari na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kutumia vizuri taaluma zao kwa kufanya njia mbadala ya kufuatilia mahudhurio ya walimu na wanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ufaulu uliyo mzuri katika Wilaya ya Kyela.

Katika suala la maadili Mhe. Manase amewataka Walimu kulinda maadili ya utumishi wa umma kwa kujiepusha na matendo maovu kama Ulevi na Ubakaji ili kulinda hadhi na Heshima katika maeneo ya kazi.

Aidha Mhe. Manase amemuagiza Mkuu wa Idara ya Afya ,Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Saumu Kumbisaga kwa kushirikiana na Wakuu wa Shule kuanza utaratibu wa upimaji mimba kwa Wanafunzi kabla ya kufunga Shule na baada ya kufungua Shule ili kutokomeza suala la mimba Shuleni.

Kwa upande wa Mtaalam kutoka NHIF Mkoa wa Mbeya Ndg.Amrani Musa Msami amesema Sekta ya Afya imeboresha huduma ya Bima za afya ikiwemo kutumia namba ya NIDA kwa Mwanachama asiye na Kadi ya Bima.

Sambamba na hilo Project Coordinator kutoka KIWIRA COAL MINE (KCM) Eng.Peter Maha amewaasa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kutumia Makaa ya Mawe kwa kupikia kama Nishati safi ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan.

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025

Kuhusu suala la udhibiti wa Magonjwa ya mlipuko hususani Ugonjwa wa Kipindupindu Mkuu wa Idara ya Afya Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Saumu Kumbisaga aliwaeleza namna ya kuchukua tahadhari Wakuu wa Shule na Walimu wakuu kujikinga na Ugonjwa huo kama Vile kunawa mikono,kutibu maji ya kunywa kwa kuweka dawa maalum.



**WAKUU WA SHULE NA WALIMU WAKUU WAKIMSIKILIZA MKUU WA WILAYA YA KYELA MHE. JOSEPHINE MANASE**

# KYELA, UMOJA WETU NDIO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## MKUU WA WILAYA YA KYELA MHE JOSEPHINE MANASE AONGOZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA (DCC) KWA AJILI YA KUPITIA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/26

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe Josephine Manase ameongoza kikao cha kamati ya ushauri ya Wilaya (DCC) kwa ajili ya kupitia mpango wa bajeti ya Mwaka wa fedha 2025/26 katika ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri tarehe 11/1/2024.

Kikao hicho kimehudhuriwa na kamati ya Ulinzi na Usalama,Watendaji wa Kata,wakuu wa Taasisi za Serikali na Dini,Wazee maarufu pamoja na Wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.

Akizungumza katika kikao hicho Mhe.Manase ameishukuru kamati ya maendeleo kwa ushirikiano katika Nyanja mbalimbali zinazopelekea shughuli za maendeleo kufanyika ndani ya Wilaya ya Kyela.

Aidha Mhe.Manase ameiomba Idara ya Kilimo kutoa Elimu kwa Wananchi juu ya uzalishaji wa Korosho pamoja na kugawa miche ya zao hilo ili kuhakikisha kilimo hicho kinarudi kama awali katika Wilaya ya Kyela.

Akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya Wanakamati waliohudhuria katika kikao hicho ikiwemo suala la ukusanyaji wa Mapato kwa Wakulima wa mpunga na changamoto katika Mfumo wa malipo ya serikali(TAUSI) Mkurugenzi Mtendaji amesema

"Ukusanyaji wa Mapato una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya Wilaya kwani 40% za Mapato zinatumika kuendeleza na kuboresha Miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Ujenzi wa Zahanati,Shule pamoja na Nyumba za Watumishi,hivyo tunatakiwa kuwa na ushirikiano thabiti katika suala zima la ukusanyaji Mapato".

Kuhusu suala la Mfumo wa Malipo ya Serikali Mkurugenzi amesema Serikali inafanya jitihada ya kuboresha mfumo huo ili kuhakikisha watumiaji wanaondokana na changamoto zinazojitokeza na kupata huduma stahiki.

Mwisho Mkuu wa Idara ya afya Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Saumu Kumbisaga ameziomba Taasisi za Dini kuhimiza Waumini wao kwenye Nyumba za Ibada juu ya kudhibiti ugonjwa hatari wa Kipindupindu kwa kuchukua tahadhari kama kula Chakula cha moto,kunawa mikono kwa kutumia sabuni na maji tiririka,Pamoja na kufanya usafi kwenye wa Mazingira yanayotuzunguka



**MKURUGENZI MTENDAJI BI. FLORAH A. LUHALA AKITOA UFAFANUZI JUU YA UMUHIMU WA MAPATO**

# KYELA, UMOJA WETU NDIO MAENDELEO YETU

UK 4

Jarida la January 2025



# RASIMU YA BAJETI YA MPANGO WA FEDHA YA MWAKA 2025/2026 YAPITA KWAKISHINDO WILAYANI

Makamu Mwenyekiti wa Halmshauri ya wilaya ya Kyela Mhe. Ambakisye Njelekela ameongoza Baraza la rasimu ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri tarehe 13/1/2025.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Katibu Tawala Wilaya ya Kyela,kamati ya Ulinzi na Usalama, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri,waheshimiwa Madiwani,Watendaji kata pamoja na wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya,Katibu Tawala Wilaya Bi.Sabrina Hamoud ameishukuru serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuleta fedha kwa ajili ya kuendeleza Miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Kyela.

Bi.Sabrina amempongeza Mkurugenzi Mtendaji kwa usimamizi mzuri wa Miradi ya maendeleo inayoleta tija kwa Wananchi na kuondokana na changamoto zinazowakabili katika Kata zao.

Vilevile Bi. Sabrina amewataka waheshimiwa madiwani na Watendaji wa Kata kukumbusha wananchi kujiandaa na uchaguzi wa madiwani,Wabunge na Raisi unaotarajia kufanyika mwaka huu.

Awali Makamu Mwenyekiti wa Halmshauri Mhe.Ambakisye Njelekela amesisitiza kuwa 40% ya ukusanyaji wa Mapato kupeleka kwa Wananchi ili ikamalize Miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela



**KATIBU TAWALA WILAYA YA KYELA BI. SABRINA HAMOUD AKITOA MAELEKEZO YA SERIKALI KWENYE BARAZA LA BAJETI**

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU

UK 5



**KAIMU AFISA MIPANGO Ndg. MOSHA MWANTOBE AKIWASILISHA RASIMU YA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KWA NIABA YA MKURUGENZI KWENYE BARAZA LA BAJETI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26 inapendekeza kukusanya na kutumia jumla ya TZS. 54,599,329,988.49 (Billioni Hamsini na Nne Millioni Miatano Hamsini na Tisa Laki Tatu Ishirini na Tisa na Mia tisa Themanini na Nane Elfu) kwa mchanganuo ufuatao:-

- Mishahara ya Watumishi walipwao na Ruzuku TZS. 32,546,086,000.00
- Miradi ya Maendeleo TZS. 12,760,664,250.00
- Mapato ya ndani TZS. 6,951,927,739.50
- Ruzuku ya matumizi mengineyo (OC) TZS. 2,340,649,998.99





**WAKUU WA IDARA NA VITENGO WAKIWA KWENYE BARAZA BAJETI LA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 13.01.2025**

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## DC KYELA AHIMIZA WATOTO WAPATE CHAKULA SHULENI

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe. Josephine Manase amefanya mkutano wa hadhara Kata ya Katumbasongwe tarehe 16.01.2025 kwa lengo la kuhamasisha upatikanaji wa Chakula Shuleni.

Aidha Mhe. Manase amewasihi Wazazi kuchangia Chakula Shuleni kwani kupatikana kwa chakula Shuleni kutapelekea kuongeza ufaulu wa Wanafunzi na kutokomeza hali ya Udumavu Shuleni.

Sanjari na hayo Mhe. Josephine Manase amewataka Wananchi kuchukua tahadhari juu Mlipuko wa Ugonjwa wa Kipindupindu kwa kunawa mikono kwa maji tiririka, kula Vyakula vya moto Pamoja na kunywa maji yaliyochemshwa.

Pamoja na hayo Mhe. Manase ametoa wito kwa Wazazi kuleta Wanafunzi Shuleni kwa lengo la kupatiwa chanjo ya kichocho pindi Wananchi watakapo tangaziwa siku maalum ya ugawaji wa chanjo hiyo.



MWANANCHI AKIUNGA MKONO HOJA YA WATOTO KUPATA CHAKULA SHULENI

Hatahivyo Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kyela ameahidi kutoa Gunia tatu(Kg 300) za Mahindi kwa Shule ya Sekondari Mwakilima, Shule ya Msingi Mwakikome Pamoja na Shule ya Msingi Katumbasongwe.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela Bi. Florah A. Luhala aliongeza kwa kusema ulaji wa Chakula Shuleni hudumisha upendo, umoja na Mshikamano baina ya Wanafunzi hivyo ni wajibu kwa Wazazi kuchangia Chakula ili watoto wapate Lishe.



MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA AKIELEZA UMUHIMU WA KUTOA CHAKULA

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



*Jarida la January 2025*



## MKUU WA WILAYA YA KYELA AHIMIZA WASIMAMIZI WA MIRADI KUMALIZAMIRADI KWA WAKATI

**Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe. Josephine Manase amefanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya Maendeleo tarehe 20.01.2025 Wilaya ya Kyela**

**Miradi iliyotembelewa ni Pamoja na Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Muungano iliyopo Kata ya Muungano. Ujenzi wa mabweni katika shule ya Sekondari Kafundo.**

**Aidha Mhe. Manase amewahi miza wasimamizi wa Miradi hiyo kuzingatia muda unaopangwa wa kumaliza Miradi hiyo ili ianze kutoa huduma kwa Wananchi.**



**MKUU WA WILAYA YA KYELA AKIKAGUA MIRADI YA MAENDELEO**



**UJENZI WA WA BWENI LA WASICHANA SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO**



# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## WANANCHI WAFURAHISHWA NA UMALIZIKAJI WA DARAJA LA IPYANA

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe. Josephine Manase ameruhusu Wananchi kuanza kulitumia daraja la Ipyana tarehe 19.01.2025 lililokuwa likifanyiwa marekebisho ndani ya siku Saba.

Aidha Mhe. Josephine Manase amewataka Wananchi kutunza Miundombinu ili iendelee kuleta tija katika jamii

Sambamba na hayo Mhe. Manase amewataka waendesha Vyombo vya usafiri ikiwemo Pikipiki, Baiskeli Pamoja na Magari kuendesha vyombo hivyo kwa umakini pindi wanapotumia Daraja hilo ili kuepusha madhara kwa wanaotembea kwa miguu hasa Wanafunzi, pia amewataka waendesha Pikipiki kushuka na kusukuma(Kukokota) Pikipiki zao katika daraja hilo.



Kwa upande wa Wananchi wa Wilaya ya Kyela wameushukuru Uongozi wa awamu ya sita unaoongozwa na mama Jemedari Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujali Hali za Wananchi wake



DARAJA LA IPYANA

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU





*Jarida la January 2025*

## DC KYELA AWATAKA WAZAZI KUWAPELEKA WATOTO WAO SHULENI KIPINDI HIKI CHA MWEZI WA KWANZA

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe. Josephine Manase amewataka wazazi katika Kata ya Muungano Kijiji cha Mwaigoga kuwapeleka watoto wao Shuleni hususani kipindi hiki cha Mwezi wa Kwanza.

Hayo yamesemwa January 21.2025 katika mkutano wa hadhara wa wakusikiliza na kutatua kero mbalimbali za Wananchi katika Kijiji cha Mwaigoga Kata ya Muungano.

Aidha Mhe. Manase ametoa onyo kali kwa Wazazi ambao watakaidi agizo la kuwapeleka watoto wao Shuleni kipindi hiki ili Watoto hao wakawasaidie kwenye shughuli za kijamii ikiwemo kupelekwa Shambani Pamoja na kwenye Biashara.

Sanjari na hayo Mhe.Josephine Manase amewaomba Wananchi kuachana na tabia ya ukataji Miti hovyo na kufukia mashimo, madimbwi pamoja na kufunika Visima vya Maji ili kuepuka athari ya vifo kwa watoto hasa tunapoelekea msimu wa Mvua.

Sambamba na hilo Mhe Josephine amewaomba Viongozi ngazi ya kata na Kijiji kwa kushirikiana na Wananchi kufanya Vikao vya mara kwa mara kwa ajili ya kujadili masuala ya maendeleo na kupeana taarifa na fursa mbalimbali zinazotangazwa na Halmashauri.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmshauri Bwn.Victor Kabuje amewataka wananchi wa Mwaigoga wenye uhitaji wa mikopo 10% unaotolewa kwa Wanawake, vijana, na wenye ulemavu kufuata vigezo ikiwemo umri, pamoja kuunda makundi ya watu (5) ili waweze kupata mikopo hiyo.

Pia Kaimu Mkurugenzi amewataka Wananchi hao kuwa waaminifu kurejesha mikopo hiyo kwa wakati pindi watakapopata ili iweze kusaidia kila mwananchi.



**WANANCHI WA KIJIJI CHA MWAIGOGA WAKIWA KWENYE MKUTANO WA HADHARA**



# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025




## MBUNGE JIMBO LA KYELA AKABIDHI GARI YA WAGONJWA (AMBULANCE) KITUO CHA AFYA CHA KILASILO

Mbunge wa Jimbo la Kyela Mhe. Ally Jumbe Mlaghila amekabidhi Gari ya Wagonjwa (ambulance) katika kituo cha Afya cha Kilasilo Kata ya Ikimba tarehe 25.01.2025.

Akizungumza katika Hafla hiyo Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe. Josephine Manase amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwakutoa gari hilo la wagonjwa katika kituo cha Afya cha Kilasilo.

Aidha Mhe. Josephine Manase ameendelea kutoa shukran nyingi kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa fedha nyingi za kutekeleza Miradi katika Sekta mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya, Miundombinu Pamoja na Kilimo na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabiri Wananchi wa Wilaya ya Kyela.

Kwa upande wake Mkuu wa idara ya Afya Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Saumu Kumbisaga ameahidi kulilinda na kulitunza Gari hilo ili liweze kuwasaidia Wananchi wa Kata ya Ikimba na Kyela kiujumla.



MKUU WA WILAYA YA KYELA MHE. JOSEPHINE MANASE KATIKA HAFLA FUPI YA KUKABIDHI GARI YA WAGONJWA



MBUNGE JIMBO LA KYELA ALLY JUMBE WAKATI AKIKABIDHI GARI YA WAGONJWA (AMBULANCE)



VIONGOZI WA CHAMA WAKIWA KATIKA HAFLA YA KUKABIDHI GARI YA WAGONJWA

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



**MKUU WA WILAYA YA KYELA MHE. JOSEPHINE MANASE AKATA KEKI NA WAFANYA BIASHARA WA SOKO LA KYELA MJINI WAKIMTAKIA HERI MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KATIKA SIKU YAKE YA KUZALIWA.**

Mkuu wa Wilaya ya Kyela Mhe.Josephine Manase kwa kushirikiana na Wafanyabiashara wa Soko kuu la Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kyela wameadhimisha siku ya kumbukizi ya kuzaliwa ya Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan tarehe 27/1/2025.

Wakiadhimisha kumbukizi hiyo Mhe. Mkuu wa Wilaya amemtakia kheri na kumshukuru Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hususani Wafanyabiashara wa Soko la Kyela.

Mhe.Manase ameupongeza Uongozi wa Soko kuu la Wilaya kwa ushirikiano mzuri na viongozi wa Serikali ili kuhakikisha biashara zinaendelea na Wananchi wanapata huduma stahiki.

Aidha, Mhe.Josephine Manase ameongeza kuwa Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameunda tume itakayotembelea kila Mkoa kukusanya maoni juu ya Kodi na Tume hiyo itakwenda kuleta muafaka juu ya Kodi wanazolalamikia Wafanyabiashara, hivyo wawetayari kutoa Maoni yao kwa Tume hiyo pindi itakapofika mkoa wa Mbeya.

Kwa upande wao uongozi wa soko kuu la CCM umemtakia kheri ya kumbukizi ya kuzaliwa Mhe. Samia Suluhu Hassan na kumpongeza kwa juhudi zote za maendeleo anazozifanya kwa ajili Watanzania







# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## KAMATI YA UCHUMI,UJENZI NA MAZINGIRA IMEFANYA ZIARA YA KUTEMBELEA NA KUKAGUA MIRADI YA MAENDELEO

Kamati ya Uchumi,Ujenzi na Mazingira imefanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya Pili tarehe 28.2.2025.

Miradi hiyo ni ujenzi wa Vyumba Viwili vya Madarasa na Matundu 8 ya Vyoo Shule ya Sekondari Bondeni inayogharimu Tsh 64,400,000, ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu katika Shule ya Msingi Sama Kata ya Ibanda ujenzi wa Vyumba Viwili vya Madarasa na Matundu 8 ya Vyoo katika Shule ya Sekondari Njisi, ujenzi huo unagharimu Tsh 64,000,000.

Wakikagua Miradi hiyo Kamati imewapongeza Wataalamu kwa kusimamia Miradi na kuwataka Wataalamu kuweka utaratibu wa kutembelea na kukagua Miradi ili kuondoa changamoto za mara kwa mara zinazojitokeza katika miradi hiyo.

Vilevile Wah. Madiwani wameomba Viongozi ngazi ya kata na Kijiji kwa kushirikiana na Mhe.Diwani wa kata ya Bondeni kufanya Vikao na kutoa Elimu kwa Wananchi wake juu ya kutoa eneo kwa ajili ya kuongeza Madarasa katika Shule ya Sekondari hiyo.

Aidha katika ukaguzi wa Bweni la watoto wenye mahitaji maalumu Shule ya msingi Sama kata ya Ibanda Mhe.Katule amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji kusimamia na kukamilisha haraka Bweni hilo hadi kufikia Tarehe 10/02/2025 Bweni hilo lifunguliwe na kuanza kutumika rasmi.

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti ameiagiza Ofisi ya Mkurugenzi kupitia Wataalamu wake ifikapo tarehe 03/02/2025 ujenzi wa Vyumba viwili vya Madarasa katika shule ya sekondari Njisi vikamilike na kuanza kutumika.

Kuhusu changamoto ya Mfumo wa Nest Mhe. Katule Kingamkono amewaomba Wataalamu kwa kushirikiana na Watendaji wa kata kutoa mafunzo kwa Wazabuni na mafundi wadogo juu ya matumizi



UJENZI WA MATUNDU 8 YA VYOO SHULE YA SEKONDARI NJISI



BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU IBANDA



UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI BONDENI

# KYELA, UMOJA WETU NDIYO MAENDELEO YETU



Jarida la January 2025



## KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO IMEFANYA ZIARA YA KUTEMBELEA NA KUKAGUA VIZUIA (MAGETI YA KUKUSANYIA USHURU)

Kamati ya fedha, Uongozi na Mipango imefanya ziara ya kutembelea na kukagua Vizuia (Mageti ya kukusanyia Ushuru) vya mapato pamoja na miradi ya maendeleo kipindi cha robo ya Pili 29.1.2025.

Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa jengo la Zahanati (OPD) Kata ya Nkuyu,maegesho ya magari Lubele kata ya Ikimba,Kizuia cha Boda Kasumulu,kizuia cha Mafiga Busale,Ujenzi wa Vyumba 4 vya Madarasa Mabweni 2 na Matundu 10 ya Vyoo Shule ya Sekondari Itope,Kizuia cha Ngeleka Kata ya Makwale na Vyanzo vya Utalii Matema.

Akikagua Vizuia vya Mapato Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri Katule G. Kingamkono amewaagiza Wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi kuweka Mkakati wa kuboresha Miundombinu maeneo ya Vyanzo vya Mapato na sehemu za Biashara ikiwemo Ujenzi wa vyoo ili kujenga Mazingira rafiki kwa wateja.

Aidha Mhe. Mwenyekiti amewataka wakusanya Ushuru na Mapato ya Halmashauri kufuata taratibu zote za ukusanyaji pamoja na kutoa Risiti kwa Wateja baada ya kupata huduma.

Hali kadhalika, katika ukaguzi wa Miradi ya maendeleo Wah.Madiwani kwanyakati tofauti wamewaomba Wataalamu ngazi ya Kata kusimamia vizuri Fedha za Miradi ya maendeleo zinazoletwa na Serikali ya awamu ya sita,inayoongozwa na Dkt Mhe: Samia Suluhu Hassan,Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kukamilisha Miradi hiyo.

Sambamba na hilo,Mhe. Mwenyekiti amewasisitiza wale wenye vigezo vya kujiunga na Mfumo wa Manunuzi (Nest) kujisajili na Mfumo huo ili kazi zao ziweze kutambulika na kufanyika kwa halali.



